KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 18, Issue 4

4th Rabiul Awwal 1433

27th Jan, 2012

HAKI ZA JIRANI YAKO [PRT I]

KULINGANA NA SUNNAH NA MFANO WA SALAF

Na: Sheikh Ali Hasan ibn Abdulhameed al-Halabi

MAJIRANI KATIKA QUR'AN TUKUFU:

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema (kama ilivyofasiriwa): **"Mwabuduni Allaah wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na masikini na jirani walio karibu na jirani walio mbali, na rafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyowamiliki mokono yenu ya kulia (kuume). Bila shaka Allaah hawapendi wenye kiburi wajivunao."** [an-Nisaa' 4:36].

Al-Imaam al-Qurtubee [katika tafsiri yake ya Al-Jaami'li Ahkaam al-Qur'an (5/183)] amesema: "Ama kumuhusu jirani, Allaah (سبحانه وتعالى) ametuamrisha katika Kitaab Chake na kwa kupitia kwa Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) yakwamba tumuhami (tumlinde), na tuheshimu haki zake na kujali kuhusu ustawi wa hali yake. Kwani hamuoni yakwamba Allaah amewataja Majirani baada ya wazazi wawili na jamaa unahusiana nao, kwani, Yeye, (سبحانه وتعالى) amesema (kama ilivyofasiriwa): **'na jirani walio karibu'** (*al-Jar Dhi'l-Qurba*), kwa maana ya wale unaohusiana nao (*Qarib*), na **'jirani walio wageni'** (*Al-Jar al-Junub*), kwa maana ya wale wasiohusiana na wewe (Gharib). Haya ni maneno ya ibn Abbaas." [Amesema al-Haafidh ibn Hajar: "at-Tabari ameipokea kwa isnaad iliyo Hasan (al-Fat-h 10/441)].

Katika lugha ya kiarabu, neno **Junub** limefasiriwa kuwa *Fulan Ajnabi* (mgeni), na neno husika ni Janabah maana yake ni **Bu'd** (mbali) - yaani kwa kuhusiana.

Wanavyuoni wa lugha ya kiarabu wamesema: "Usinizuiye kumuona Na'il kwa sababu ya Janabah (yaani - kwa kuwa sina uhusiano nae), kwani mimi ni mtu ambaye katikati ya halaiki ya watu ni Ghareeb (mgeni)."

Mshairi, al-Ash'aree amesema: "Mimi nimekuja kumtembelea Hurayth licha ya kuwa ni janabah kwake (sina uhusiano nae), lakini hakunipa chochote (yaani, kwa sababu ya kutohusiana nae).

Amesema al-Qurtubi (رحمه الله): "Juu ya msingi huu, uhusiano na majirani ni uwajibikaji wa ki-Dini, bila ya kujali iwapo ni Waislamu au Makafiri, na hii ni rai yenye nguvu tena iliyo swaheeh."

Ihsaan (kutenda wema), inaweza kumaanisha kumfariji, kuwa mkarimu kwake, kujiepusha na kumsumbua, na kumtetea."

Al-Haafidh ibn Hajar amesema: "Maana ya *Al-Jar al-Qarib* ni wenye kuhusiana kwa damu, na maana ya *al-Jar al-Junub* ni wale wasiohusiana hivyo. Hii ni rai ya wanavyuoni wengi ... Wengine wamesema yakwamba *Al-Jar al-Qarib* inawahusu Waislamu na *al-Jar al-Junub* inawahusu wasiokuwa Waislamu, au kwamba *Al-Jar al-Qarib* inamuhusu mke wa mtu, na *al-Jar al-Junub* inawahusu wenzako unaosafiri nao." [Fat-h al-Baari (10/441)].

UFAFANUZI WA "JIRANI"

"Neno *Jar* (Jirani) linawahusu wote wawili, Waislamu na Makafiri, walio na misimamo ya dini na wasiokuwa na misimamo ya dini, Marafiki na Maadui, wananchi wenzako na wageni, wenye kukutendea wema na wenye kukudhuru, jamaa zako na wageni usiowajua, wenye nyumba zilizo karibu na kwako na wenye nyumba za mbali na kwako."

Majirani wamegawanyika kwenye mafungu chungu nzima. Yaliyo bora miongoni mwayo ni wenye kukusanya sifa [zenye kupendekeza] zilizotajwa hapo juu, na zenye kufuata kwa ubora ni zenye kuwa na sifa hizi, na namna hiyo hadi kuwafikia majirani wenye angalau sifa moja ya hizi. Majirani waovu ni wale wenye kukusanya sifa zote mbaya. Kila jirani hupewa haki kulingana na fungu alimo ndani yake. Ikiwa jirani huonyesha sifa zote mbili, nzuri na mbaya, itatulazimu kupima ni zipi zilizozidi nyengine baina ya nzuri na mbaya, kisha nasi tumlipe kulingana na alivyo [Fat-h al-Baari (10/442)].

MASAFA YENYE KUSTAHIKI UJIRANI

Wamekhitilafiana wanavyuoni kuhusu mas'ala ya ufafanuzi na masafa ya "Ujirani."

Wamesema, Al-Uza'i na ibn Shihaab: "Nyumba arubaini kwa kila upande."

Ali ibn Abu Twaalib amesema: "Kila mwenye kusikiya muadhini ni jirani."

Baadhi ya wanavyuoni wamesema: "Kila mwenye kusikiya Iqaamah (ulinganizi unaoletwa pindi tu muadhini umalizikapo, unaolinganiwa ndani ya mskiti badala ya kwenye vinara vya mskiti) ni jirani wa mskiti huo."

Wanavyuoni wengine wamesema: "Yoyote mwenye kuishi na mtu kwenye kijiji au mji ni jirani."

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema (kama ilivyofasiriwa): **"Kama wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao na watangazao uovu mjini hawataacha (visa vyao hivyo vya upotofu), kwa yakini tutawasalitisha (Tutakuondokesha) juu yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda kidogo tu; (kisha litawafika la kuwafika)."** [al-Ahzaab 33:60].

Kwahiyo Allaah (سبحانه وتعالى) amefanya kuwepo kwa wanafiki mjini Madinah kuliwafanya wao kuwa ni Majirani wa Mtume (صلى الله عليه وسلم).

YALIYOMO

HAKI ZA JIRANI YAKO 1 - 4

TANGAZO LA DARSA- MAZRUI 4

Majirani wamegawanyika kwenye mafungu tafauti; wa karibu mno ni mke wa mtu, kama ulivyo msemo; *Aya Jarata Bini fa-in-naka Taliqah* ("Ewe Jirani - yaani Mke wangu - niondokee kwani nishakuacha) [Tafseer al-Qurtubi (5/185)].

Amesema ibn Hajar: "Amepokea Ibn Wahb kutoka kwa Yunus kutoka kwa ibn Shihaab: Nyumba arubaini kwenye upande wako wa kulia, wa kushoto, nyuma yako na mbeleni kwako." [al-Fath (10/447). **Hadeeth hii imekuja chini ya kichwa** Haq al-jiwar fi Qurb al-Abwab (**Haki za Majirani wenye milango iliyokurubiana**)].

Al-Halimi amesema katika Shu'ab al-Iman (3/358): "Ama kumuhusu mwenzio unaesafiri nae, basi yeye ni jirani kwa sababu ana ushirika katika nafasi ya mwenye kusafiri, na washirika katika usafiri huwa na mambo mengi ya kubadilishana, kama ilivyo hali ya Majirani kwenye soko moja au mtaa. Hii ndiyo sababu ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) ametuamrisha kumjali jirani yako (yaani: Jirani msafiri). Na Allaah Ndiye Mjuzi Mkubwa.

MASIMULIZI NA MASHAIRI JUU YA HAKI ZA MAJIRANI

Katika Uislamu, Majirani wamepewa daraja ya juu kabisa, kinyume cha mifumo mengine ya ki-utawala na sheria za kutungwa na wana-adamu. Kwa hakika, mifumo hii mengine inawahimiza watu wasiwaheshimu majirani zao, ili iwe ni urahisi kwa kuwaingilia kwenye haki zao na kuwakandamiza.

Nyimbo za kileo zilizo maarufu zenye kumsifu jirani aliyeonekana kwenye dirisha, na mfano wa hayo, zimetangaa baada ya kupoteza imani zetu na sifa za uungwana, na tukaanza kuwaiga mababu zetu ki-Upofu, na tukajisalimisha kwa ubepari wa kimila. Tumefikia katika hali ambapo kijana yoyote aliye na akili mbovu miongoni mwetu anaweza kuimba nyimbo za mapenzi kumuhusu jirani (mwanamke) mambo ambayo hata katika zama zetu za jaahiliyyah hazikuwahi kuwepo, licha ya kwenye zama za Uislamu. Kwa hakika, mshairi wetu aliyekuwa bingwa, 'Antar alikuwa akistahi heshima za wengine, na pindi akutanapo na jirani yake mwanamke alikuwa akisema:

"Naangusha macho yangu pindi anitokezeapo jirani yangu (mwanamke), mpaka aingie nyumbani mwake." ['Antarah, Diwan, Uk.308].

Uislamu umetuhimiza tushikamane na kiwango hichi cha tabia nzuri. Kuna Ayaat nyingi sana, ahaadeeth na riwaya zinazoshughulikia uhusiano na majirani, kulinda heshima zao, kuficha au kusitiri makosa yao au kuteleza kwao, kuwasaidia kwenye nyakati za shida, kujiepusha na kuwatazama wanawake zao, na kujiepusha na kufanya jambo lolote liwezalo kuwatia shaka au kuwaudhi." [Muhammad 'Ali al-Hashimi Shakhsiyah al-Muslim, Uk.178-9].

Zaidi ya hayo, Washairi na Wanavyuoni wa ki-Islamu wameandika kuhusu haki na ulinzi wa Majirani, miongoni mwao ni hizi tulizoziandika:

- ◊ Wewe ni Jirani yangu na ufurahie wema wa Ujirani.
- ◊ Mimi nimewajibika kudumisha haki za Jirani yangu.
- ◊ Pindi Jirani yangu aondokapo, huangaza jicho langu kwa niaba yake.
- ◊ Kwa kulinda mambo yake ya faragha na siri.
- ◊ Hapana tafauti yoyote kwangu iwapo mlango wake umefungwa au uwazi.
- ◊ Namwambia Jirani yangu, ikiwa atakuja kulalamika kwangu.
- ◊ Bila ya kujali iwapo anasema ukweli au anadanganya,
- ◊ Ikiwa wema nilokufanyia haujakufikia, ingawa wewe ni jirani yangu,
- ◊ Basi kwa hakika ubaya wangu niloufanya hautokufika."
- ◊ Wamenilaumu kwa kuiuza nyumba yangu kwa bei rahisi,
- ◊ Lakini hawakuujua usumbufu nilioupata kwa jirani yangu.
- ◊ Nikawaambia musinilaumu,
- ◊ Kwani thamani ya nyumba inategemea majirani. [**Ibn Muflih**, al-Adab al-Shariyyah wa'l-Minah al-Mar'iyyah (2/15-16)].

Al-Qatani amesema katika Nuniyyah yake (Uk.42).

- ◊ Zilinde haki za Jirani yako,
- ◊ Kwani kila Jirani-Muislamu ana haki mbili, [yaani haki ya Uislamu na haki ya Ujirani]
- ◊ Kuhusiana na Jirani Mjinga, imesemwa:
- ◊ Hana analotamani kutoka kwa Jirani yake isipokuwa ni kuwachana nae. [Siyar A'lam an-Nubalaa' (4/552), **imepokewa kutoka kwa Wahb ibn Munabbih**].

Amesema ibn Abdul-Barr:

"Kuna sifa tatu ambazo, iwapo zitapatikana kwa mtu, basi hapana shaka yakwamba yeye ni mtu mzuri mwenye akili timamu:

- ◊ Akisifiwa na Jirani yake,
- ◊ Akisifiwa na Jamaa zake, na
- ◊ Akisifiwa na Rafiki zake.

Mambo matatu hufanya maisha kuwa magumu:

- ◊ Jirani muovu,
- ◊ Mtoto mkorofi na
- ◊ Mke mwenye tabia mbaya asiyekuwa na busara.

Kutoka kwa Hasan ibn 'Isa an-Naisaburi: "Nilimuuliza Abdullaah ibn al-Mubaarak: Mtu mmoja alinijia na malalamiko kuhusu njambo alilolifanya mfanyi kazi wangu, na mfanyi kazi wangu akakanusha madai hayo. Singelipenda kumuadhibu iwapo hakuwa na hatia yoyote, lakini singelipenda kumuacha huru kwa vile jirani yangu atanikasirikia. Sasa nifanyeje?

[Abdullaah ibn al-Mubaarak] akasema: "Labda huwenda mfanyi kazi wako anastahiki kuadhibiwa kwa jambo alilolifanya, kwahiyo tafakari hilo. Jirani yako anapolalamika kumuhusu yeye, basi muadhibu kwa ulilo na hakika nalo kuwa amefanya, ili upate kumtosheleza Jirani yako na umuadhibu mfanyi kazi wako kwa aliyoyafanya." [**Al-Khara'iti**, al-Muntaqa min Makarim ul-Akhlaq (No.101), **imenukuliwa na as-Salafi**].

Na imesemwa:

- ◊ "Moto wangu na moto wa Jirani yangu ni mmoja,
- ◊ Yeye ndiye apewae Sufuria mwanzo.
- ◊ Mimi sijali yakwamba mlango wake hauna pazia." []**Ibn Qutaybah**, 'Ayun al-Akhbar (2/193).

HAKI NA FADHLA ZA MAJIRANI KULINGANA NA SUNNAH ZA MTUME (صلى الله عليه وسلم)

1. UHARAMU WA KUWADHURU JIRANI ZAKO.

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه); Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Hatoingia Peponi, yule ambaye Jirani yake hakusalimika na tabia zake mbovu." [Al-Bukhari (6016), Muslim (46). Riwaya kama hiyo imepokewa na Ahmad (3/154), al-Haakim (1/11) na ibn Hibban (510) kwa isnad swaheeh kutoka kwa Anas (رضي الله عنه). Riwaya ya tatu imetolewa na al-Bukhari (6016) kutoka kwa Abu Sharih al-Ka'bi. Kuna riwaya nyingi kama hizo zenye isnad nyingi kwenye Mlango huo huo.]

2. MAPENDEKEZO YA KUWATENDEA WEMA MAJIRANI

Kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) aliyesema: "Amesema Mtume (صلى الله

عليه وسلم): 'Jibril hakuacha kunisisitiza kumtendea wema Jirani mpaka nikadhania yakwamba ataniambia nimfanye kuwa ni miongoni mwa warathi wangu." [al-Bukhari (6014), Muslim (2624). Vilevile angalia; al-Bukhari (6015), Muslim (2625), kutoka kwa ibn 'Umar na wengineo ambao ni wingi sana kuwanukuu hapa].

3. MWENYE KUMDHURU JIRANI YAKE NA ALA'ANIWE.

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtu mmoja alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kumshitakia kuhusu jirani yake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia mara tatu, "Fanya subira", kisha katika mara ya tatu au ya nne, akamwambia: "Nenda ukaweke vyombo vyako njiani, kwahiyo yule mtu akafanya hivyo. Mara wapita njia wakaanza kumuuliza yule mtu kutaka kujua kunaendelea nini, nao wakaambiwa, "Amedhuriwa na jirani yake", basi watu wakaanza kusema, "Mungu atamlaani!" Yule Jirani akatoka nje na akamwambia yule mtu, "Haya basi rudisha vyombo vyako, kwa hakika naapa kwa Jina la Allaah, mimi sitokudhuru tena." [Abu Daawud (5153), *al-Bukhari al-Adab al-Mufrad* (124), Al-Haakim (4/160), kwa isnad iliyo Hasan. Kuna yanayofanana na hayo kutoka kwa Abu Juhayfa, imepokewa na al-Bazzar (1903), al-Haakim (4/166), na al-Bukhari katika al-Adab al-Mufrad (125), lakini kuna udhaifu fulani na mpokezi mmoja au wawili kwenye isnad yake].

4. KUWASHUGHULIKIA MAJIRANI.

Kutoka kwa Abu Dharr (رضي الله عنه) aliyesema; "Rafiki yangu kipenzi (yaani:Mtume (صلى الله عليه وسلم)) ameniusia mimi: "Kila upikapo mchuzi, ongeza maji zaidi kidogo, kisha nenda ukatafute nyumba iliyoko jiranini mwako na uwape nao kwa ukarimu" [Muslim (2625, 143). Vilevile angalia kwenye al-Bazzar (1901); at-Twabaraani: *al-Awsat na Al-Majma'* (8/165), kutoka kwa Jaabir kwa isnad yenye udhaifu khafifu] Katika riwaya nyengine: "... Ewe Abu Dharr, kila upikapo mchuzi, zidisha maji ndani yake, na uwakumbuke majirani zako." [Muslim (2625,142)] Na katika riwaya nyengine: "... Ili upate wa kuwatosha jamaa zako na Majirani zako." [Ibn Hibban (513), na Ahmad (15/156), kwa isnad iliyo swaheeh]

5. KUWA MSHIRIKA KWA JIRANI ZAKO

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه); Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Asimkataze mmoja wenu jirani yake asiegemeze mbau zake kwenye ukuta wake." [al-Bukhari (2463) na Muslim (1609). Riwaya kama hiyo imesimuliwa na Ahmad (3/479, 480) na Ibn Maajah (2336), kutoka kwa *Mujamma' ibn Jaryah;* na nyengine kutoka kwa Ibn Abbaas; angalia Ahmad (1/303) na al-Bayhaqee (6475)].

6. KUJIEPUSHA KUMDHURU JIRANI YAKO NI KATIKA SEHEMU YA IMANI

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه); kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba amesema: "Yoyote mwenye kumuamini Allaah na Siku ya Mwisho na asimdhuru Jirani yake." [al-Bukhari (6475) na Muslim (47, 74)]

7. JIRANI ALIYE BORA

Kutoka kwa Abdullaah ibn 'Amr (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Rafiki aliye bora, mbele ya Allaah, ni yule aliye bora kwa rafiki yake, na Jirani aliye bora, mbele ya Allaah, ni yule aliye bora kwa Jirani yake." [at-Tirmidhee (1944), Ahmad (2/167), ad-Daarimi (2/215) na al-Haakim (1/164) kwa isnad iliyo swaheeh]

8. HAKUNA 'AMALI YOYOTE YENYE KUMDHURU JIRANI ICHUKULIWAYO KUWA NI KHAFIFU

Kutoka kwa 'Abdah ibn Ali Lubabah (رحمه الله) aliyesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Hakuna 'amali yoyote yenye kumdhuru jirani ichukuliwayo kuwa ni khafifu." [Marejeo yapatikanayo kwenye [*ad-Durr al-Manthur* (2/159) yakuwa "imepokewa kutoka kwa Abu Lubabah" ni makosa.

9. JIRANI MWEMA HUCHANGIA KUNAKO FURAHA

Kutoka kwa Sa'd ibn Abi Waqqas (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: 'Mambo manne ni yenye kuchangia kwenye furaha: Mke mwema, nyumba yenye nafasi kubwa, jirani mwema na chombo kizuri cha usafiri. Na mambo manne ni yenye kuchangia kwenye mateso: Jirani muovu, mke muovu, nyumba yenye nafasi ya dhiki na chombo kibaya cha usafiri.' [Ibn Hibban (1232), na al-Khatib (12/99) kwa isnad iliyo swaheeh]

10. KUWATENDEA MAJIRANI WEMA

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه); Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Kuwa Mcha Mungu na utakuwa ni mbora wa wanaofanya 'Ibada miongoni mwa watu. Tosheka na fungu lako: utakuwa ni mwenye shukrani zaidi miongoni mwa watu. Wapendelee watu yale unayojipendelea nafsi yako: utakuwa ni Mu'min. Mtendee jirani yako mazuri: utakuwa Muislamu. [Ibn Maajah (4217), Abu Ya'la (5865) na Abu Nu'aym: *al-Hilya* (10/365). Kuna baadhi ya udhaifu kwenye isnad yake. Riwaya inayofanana nayo yapatikana kwenye *Ar-ba'i ad-Da'wah wa-d-Du'ah, No.13*]

11. MADHAMBI YA KUMUUDHI JIRANI NI MIRUNDIKO

Kutoka kwa Abu Zabyah al-Kala'i, aliyesema: Nilimsikiya al-Miqdad ibn al-Aswad akisema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwauliza watu kuhusu uzinifu, nao wakamjibu kwa kusema: "[Ni] Haraam; Allaah na Mtume wake wameharamisha."

Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Kwa hakika, mtu kuzini na wanawake kumi ni madhambi sahali kwake kuliko kuzini na mke wa jirani yake."

Akasema [al-Miqdad]: [Mtume (صلى الله عليه وسلم)] akawauliza kuhusu wizi (kuiba). Wakamjibu: [Ni] Haraam; Allaah na Mtume wake wameharamisha."

Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Kwa hakika, mtu kuiba kwenye nyumba kumi ni madhambi sahali kwake kuliko kuiba kwenye nyumba ya jirani yake." [Ahmad (6/8), al-Bukhari; *al-Adab al-Mufrad* (103), na at-Twabarani: *al-Kabir* (20/210/605), kwa isnad nzuri (jayyid), al-Haafidh amesema yakwamba Abu Zaybah ni Maqbul (anaekubalika), lakini kwa hakika amepangwa kuwa ni muaminifu na ibn Mu'in na wengineo].

12. USILE UKASHIBA HALIYAKUWA JIRANI YAKO ANA NJAA [Hiki ni kichwa kilichotumiwa na al-Bukhari katika *al-Adab al-Mufrad* (Uk.1/194)]

Kutoka kwa Abdullaah ibn Musawir aliyesema: "Nilimsikiya Ibn Abbaas akimtaja Ibn az-Zubayr, akisema yakwamba alikuwa ni mtu bakhili, kisha akasema: 'Nimemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: 'Si Mu'min mwenye kushiba haliyakuwa jirani yake aliye karibu nae akiwa na njaa.'

NUKTA MUHIMU: Hadeeth hii inaleta ishara iliyo wazi yakwamba ni Haraam kwa mwenye uwezo (tajiri) kuwaacha majirani zake wakiwa na njaa. Ni lazima ajitolee kwao kitu chochote kiwezacho

kuizuia njaa hiyo, na chochote kiwezacho kuwasitiri iwapo watakuwa hawana mavazi, na mahitaji mengine kama hayo." [al-Silsila as-Swaheehah (1/230)]

13. SI MU'MIN YULE ASOMPENDA JIRANI YAKE

Kutoka kwa Anas (رضي الله عنه); kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Naapa kwa Ambaye roho yangu imkononi mwake, haamini yoyote ki-kweli kweli mpaka ampendelee jirani yake—au ndugu yake—lile ajipendelealo nafsi yake." [Muslim (45, 72)]

14. NASWIHA KWA WANAWAKE WASIDHARAU TUNU ZITOKAZO KWA JIRANI

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema; Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisema: "Enyi Wanawake wa ki-Islamu! Hapana ruhusa ya yoyote kuidharau tunu ya Jirani yake, hata kama ni mguu wa kondoo [tu]. [al-Bukhari (6017) na Muslim (1030). Maana yake ni kwamba, hairuhusiwi kwa yoyote kuidharau tunu itokayo kwa jirani yako, hata kama ni kitu maalum kisichofaa au kisichokuwa na thamani (al-Fat'h 10/445)]

15. HAKI ZA MAJIRANI WENYE MILANGO ILIYOKURUBIANA [Hiki ni kichwa kilichotumiwa na al-Bukhari katika swaheeh yake (Fat'h 10/447)]

Kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) aliyesema: "Nilisema: Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi nina Majirani wawili, ni yupi kati ya hao wawili nimkusudie zawadi?" Akanijibu Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mkusudie jirani ambaye mlango wake uko karibu na wako." [al-Bukhari (6020)]

16. KUTAFUTA HIFADHA KWA ALLAAH (سبحانه وتعالى) KUTOKAMANA NA JIRANI MBAYA

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه): Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisema: "Yaa Allaah, najikinga Kwako kutokamana na Jirani muovu katika mazingira ya nyumba yangu ya kudumu, kwani jirani kwenye jangwa hubadilika daima." [Hadeeth iliyo swaheeh; angalia nukta zangu juu ya *al-Tuhfah an-Nadiyyah bi Sharh al-Lamiyyah al-Wardiyyah* (sehemu ya 56), hivi sasa kiko kwa mchapishaji.]

17. UGOMVI NA MAJIRANI

Kutoka kwa 'Uqbah ibn 'Amir (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyesema: "Makundi mawili ya kwanza yatakayopingana katika Siku ya Kufufuliwa yatakuwa ni Majirani wawili." [at-Twabarani; al-Kabir (836, 852), na Ahmad (4/151), kwa isnad mbili kutoka kwa Abu 'Ush-Shanah kutoka kwake kwa isnad iliyo swaheeh. Al-Haythamee ameiorodhesha kwenye daraja ya Hasan katika *al-Majma'' (*10/349), al-Mundhiree ameiorodhesha kuwa *jayyid* katika at-Targheeb (3/355)]

18. KUMDHURU JIRANI HUWENDA IKAPELEKEA KUNAKO MOTO WA JAHANNAM

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtu mmoja aliuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allaah! Kuna mwanamke anayeswali, na kutoa swadaka na kufunga sana, lakini alikuwa akiwadhuru Jirani zake kwa maneno yake [kwa kuwatukana]."
Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Huyo Atakwenda Motoni."
Mtu akasema: "'Ewe Mjumbe wa Allaah! Kuna mwanamke [mwengine] aliye maarufu sana na kujulikana kwa jinsi anavyoswali na kufunga kwa uchache, lakini yeye hutoa swadaka kutokamana na Maziwa ya kuganda anayoyafanya [*al-Awthar min al-Aqit*], lakini yeye hawadhuru Jirani zake."
Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Huyo atakwenda Peponi." [Ahmad (2/440), Ibn Hibban (2054 - az-Zawaa'id) na al-Haakim (4/166), kutoka kwa Abu Yahya mtumwa wa Ja'dah; isnad yake ni swaheeh]

19. KUCHUKULIA KERO LA MAJIRANI KWA KUSUBIRI

Kutoka kwa Abu Dharr (رضي الله عنه) aliyesema; Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Kuna watu sampuli tatu ambao Allaah anaowapenda ... [mmojawapo ni] ni yule mwenye Jirani anaemuudhi, lakini yeye akawa ni mwenye kuyachukulia maudhi hayo kwa kusubiri, mpaka kifo kikawatenganisha kwa kuondoka mmoja wao."

20. USHAHIDI WA MAJIRANI

Kutoka kwa Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtu mmoja alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Nitajijuaje mimi iwapo nimefanya sawa au nimekosa?" Akamjibu: 'Uwasikiapo Majirani zako wakisema kuwa umefanya uzuri, basi utakuwa umefanya uzuri, na uwasikiapo Majirani wakisema kuwa umefanya makosa, basi utakuwa umefanya makosa." [Ahmad (1/402), Ibn Maajah (4223), Ibn Hibban (526) na al-Bayhaqee (3490) kwa isnad iliyo swaheeh. Hadeeth hii vilevile imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah: al-Haakim (1/375) na al-Isbahani, at-Targhib (844)]

21. FITINA ZA MAJIRANI

Kutoka kwa Hudhayfah (رضي الله عنه) aliyesema: Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Madhambi ya mtu (Fitina) yanayohusiana na mkewe, mali yake, watoto wake na Jirani yake yanaweza kufidiwa na swala, saumu, kutoa swadaka, na kuamrisha mema na kukataza maovu ..." [al-Bukhari (525) na Muslim (144)]

22. KUWAPA JIRANI ZAKO SWADAKA

Kutoka kwa Abu Sa'id al-Khudhree (رضي الله عنه) aliyesema: Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Swadaka hapewi tajiri, lakini hupewa kwa wale wenye kuipigania njia ya Allaah, kwa mpita njia, au kwa jirani yako aliye masikini, ambae [mara nyengine] akupae zawadi au akualikae nyumbani kwake." [Abu Daawud (1635, 1636), Ibn Maajah (1841), Ibn al-Jarud (365), Ibn Khuzaymah (2374), al-Haakim (1/407), al-Bayhaqee (7/13), Ahmad (3/56) na Abdul-razzaq (7151), kutoka kwa Zayd ibn Aslam, kutoka kwa 'Ataa' kutoka kwake, isnad yake ni swaheeh. Palikuwa na shaka kuihusu hadeeth hiyo, lakini haikuwa kwenye kiwango cha kukataa uswaheeh wake].

23. KUSHIRIKIANA NA MAJIRANI

Kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) aliyesema: "Wallaahi, tulikuwa tukiuona mwezi kongo, miezi kongo mitatu katika muda wa miezi miwili, na hapakuwepo na moto [utokanao na mapishi] kwenye nyumba ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). [Mpokezi wa hadeeth hii] akasema: "Ewe shangazi! Muliishi kwa kitu gani? Akamjibu: Vitu viwili vyeusi: Tende na maji. Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na Majirani wa ki-Answari waliokuwa na mifugo, na walikuwa wakimletea Mtume (صلى الله عليه وسلم) maziwa, nae alikuwa akitupa na sisi maziwa hayo tunywe." [AL-Bukhari (2567) na Muslim (2972)]

TANGAZO LA DARSA MASJID MAZRUI

Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alkhamisi na Jumamosi. Darsa zote ni baina ya Maghrib na 'Ishaa'. Nyote munaalikwa kuhudhuria.